# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani, Buyu,
70490 Mjini Magharibi,
S.L.P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 2242000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA KAMATI YA BAJETI KUHUSU MAJUMUISHO YA MIJADALA YA BAJETI ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

### UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi tukaweza kupitisha bajeti za Wizara zote ishirini (20). Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Waheshimiwa Wenyeviti wa Baraza kwa uongozi wenu thabiti na weledi mnaoendelea kuutoa katika kuendesha shughuli za Baraza hili Tukufu. Hekima na busara zenu zimewezesha mijadala ya Baraza kuendeshwa kwa utaratibu, uwazi na ufanisi, hali inayotuwezesha sisi Wajumbe kutekeleza ipasavyo majukumu yetu ya Kikatiba ya kuidhinisha Bajeti kwa niaba ya wananchi tunaowawakilisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati ya moyo wangu, napenda kutumia fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake thabiti, wenye maono na uliojaa busara. Uongozi wake umeendelea kutoa mwelekeo sahihi katika kusimamia rasilimali za nchi yetu, kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma na kusukuma mbele ajenda za maendeleo, jambo lililochangia kwa kiasi kikubwa kuimarika kwa uchumi, ustawi wa wananchi wa Zanzibar kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kipekee kabisa naomba nitumie fursa hii kutoa pongezi za dhati kwa Makamo wa Pili wa Rais pamoja na Mawaziri wote kwa kuwasilisha kwa ufanisi hotuba za bajeti za wizara zao katika Baraza lako tukufu, sambamba na kutoa ufafanuzi wa kina kwa hoja na maswali ya Wajumbe, hatua iliyowezesha kuimarisha uelewa na hatimaye kuidhinishwa kwa bajeti hizo kwa mafanikio. Vilevile, nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe kwa kutekeleza kwa weledi na uzalendo

mkubwa majukumu yao ya kupitia, kujadili na kuidhinisha bajeti za Wizara na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Shukrani za kipekee na za dhati naziwasilisha kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti, ambao kwa umahiri wao, uzoefu na weledi mkubwa wameendelea kutoa mchango muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Kwa kutambua mchango wao mkubwa katika kufanikisha shughuli za Kamati hii, naomba uniruhusu niwatambue kwa majina yao kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Ali Suleiman Ameir | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Maryam Said Khamis | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Bakar Hamad Bakar | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Farida Amour Mohammed | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Mohammed Ali Salim | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Sulubu Kidongo Amour | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Yussuf Ali Hassan | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** Napenda pia kutumia nafasi hii kuishukuru na kuipongeza Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti kwa kuhakikisha shughuli za Kamati zinafanyika kwa ufanisi na utaratibu unaostahili. Weledi na ushauri wao wa kitaalamu umechangia kwa kiasi kikubwa kwa Kamati kutekeleza majukumu yake kwa umakini, weledi na kwa ufanisi mkubwa. Kwa ruhusa yako Mheshimiwa Spika, naomba niwatambue kwa majina yao kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Asha Said Mohamed | Katibu |
| 2. | Ndg. Maryam Mohammed Othman | Katibu |
| 3. | Ndg. Shaib Fadhil Shaib | Katibu |
| 4. | Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi | Katibu |
| 5. | Ndg. Said Bakar Hamad | Msaidizi wa Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa hotuba hii ni matakwa ya Kanuni ya 113(2) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2024, ambayo inaielekeza Kamati ya Bajeti kwa kushirikiana na Serikali kufanya majumuisho kwa ajili ya kuzingatia hoja zilizojitokeza wakati wa mjadala wa Bajeti za Wizara. Aidha, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 113(3) ambayo inampa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti fursa ya kuwasilisha mbele ya Baraza hili tukufu Hotuba ya Majumuisho kabla ya

kuwasilishwa kwa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo pamoja na Makadirio ya Bajeti ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya utangulizi huo, sasa naomba kuwasilisha Hotuba ya Kamati ya Bajeti kuhusu Majumuisho ya Mjadala wa Bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Hotuba hii inawasilisha hoja za kibajeti zilizohitaji ufafanuzi zaidi, pamoja na majibu ya Serikali na ushauri wa Kamati ya Bajeti. Aidha, baadhi ya hoja zilichangiwa na Wajumbe wengi kutokana na umuhimu wake kwa wananchi na maendeleo ya nchi yetu, huku nyingine zikichangiwa kwa hisia na msisitizo mkubwa.

## UFAFANUZI WA HOJA ZILIZOJADILIWA WAKATI WA KIKAO CHA MAJUMUISHO BAINA YA SERIKALI NA KAMATI YA BAJETI

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kukamilika kwa mchakato wa mjadala na uidhinishaji wa Bajeti za Wizara katika Baraza lako Tukufu, Kamati ya Bajeti ilifanya kikao cha majumuisho na baadhi ya Wizara kwa lengo la kupata ufafanuzi wa ziada kuhusu hoja za kibajeti zilizohitaji maelezo zaidi. Katika kikao hicho, jumla ya hoja nne (4) kutoka Wizara ya Kazi na Uwekezaji pamoja na Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji zilijadiliwa.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kurahisisha uelewa wa hoja hiyo, imewekwa katika mfumo wa jadweli lililogawanywa katika sehemu tatu. Sehemu ya Kwanza inaonesha hoja iliyoibuka, Sehemu ya Pili inaeleza majibu yaliyotolewa na Wizara husika, na Sehemu ya Tatu ni maoni pamoja na ushauri wa Kamati kuhusu hoja hiyo.

JADWELI: HOJA ZILIZOIBUKA

| WIZARA YA KAZI NA UWEKEZAJI | | | |
|---|---|---|---|
| **SNo.** | **HOJA ZILIZOIBUKA** | **MAJIBU YA WIZARA** | **MAONI YA KAMATI** |
| 1. | Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Kazi na Uwekezaji iliidhinishwa TZS 28,700,300,000. Aidha, kutokana na mabadiliko ya muundo mpya wa Serikali Wizara ya Kazi na Uwekezaji ilibakishiwa TZS 27,750,285,000. Pia Serikali ikatoa TZS 977,787,273 kuzipeleka kwenye Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji. Jumla ya fedha zote ni TZS 28,728,072,273. Hii inafanya kuwepo kwa ongezeko la TZS 27,772,273. Ili Wizara hizi ziweze kutekeleza Bajeti zake kwa ufanisi, inapaswa kubainishwa ongezeko hili litakuwepo katika Bajeti ya Wizara gani kati ya Wizara ya Kazi na Uwekezaji na Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji. | Katika Mwaka wa Fedha 2025/26, Wizara ya Kazi na Uwekezaji iliidhinishiwa jumla ya TZS 28,700,300,000/=. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya muundo mpya wa Mawizara hadi kufikia kipindi cha miezi tisa, Fungu la Wizara ya Kazi na Uwekezaji lilipunguziwa bajeti ya TZS 977,787,273/= kwenda Fungu la Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji. Kwa mantiki hiyo, hadi kufikia tarehe 31 Machi 2026 bajeti halisi iliyobakia katika Fungu la Wizara ya Kazi na Uwekezaji ni TZS 27,722,512,727/= badala ya TZS 28,750,285,000/= ambazo pesa hizo katika OC kupitia Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kazi na Uwekezaji. | Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa katika nyaraka za bajeti na taarifa za utekelezaji wa bajeti zitakazowasilishwa katika Baraza na Kamati zinaonesha kwa uwazi kiasi cha fedha kilichohamishwa kutoka fungu moja kwenda jingine, bajeti halisi iliyobaki katika kila Wizara baada ya marekebisho, pamoja na athari za mabadiliko hayo katika utekelezaji wa shughuli zilizopangwa. Hatua hii itasaidia kuimarisha uwajibikaji, uwazi na uelewa sahihi wa matumizi ya fedha za umma. |
| **WIZARA YA VIJANA, AJIRA NA UWEZESHAJI** | | | |
| **SNo.** | **HOJA ZILIZOIBUKA** | **MAJIBU YA WIZARA** | **MAONI YA KAMATI** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kufuatia mabadiliko ya muundo mpya wa Serikali, Serikali ilipeleka jumla ya TZS 1,678,696,982.70 kwa Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji. Wakati wa uwasilishaji wa makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara hiyo iliwasilisha utekelezaji wa TZS 20,419,108,690 bilioni. Kati ya fedha hizo, TZS 16,500,000,000 bilioni ziliripotiwa kama utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotokea Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo. Kamati inaomba ufafanuzi wa Ongezeko la TZS 2,240,411,707.30. | Bajeti ya TZS 20,419,108,690 ni fedha za bajeti zilizohamishiwa kutoka Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo na Wizara ya Kazi na Uwekezaji kwa Mwaka 2025/2026 kwenda Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji. Bajeti hiyo inajumuisha Mishahara, Matumizi ya Kawaida (OC) pamoja na Miradi ya Maendeleo. Bajeti hiyo ilipangwa katika programu za Wizara hizo mbili ambazo zimeunda Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji. Aidha, Jumla ya TZS 1,678,696,982.70 zilizoingizwa kutoka Serikalini ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida pekee. Fedha hizi hazijajumuisha mishahara ya wafanyakazi ambazo bajeti yake ni TZS 1,133,095,000 na zitalipwa kupitia Wizara wanazotoka watumishi hao ambapo bajeti yake inaonekana katika Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji. Hivyo, fedha inayoonekana kama ni ongezeko TZS 2,240,411,707.30 si ongezeko bali inajumuisha mishahara ya wafanyakazi na matumizi mengine ya | Kamati inaishauri Serikali kui kuhakikisha taarifa za fedha zinapohamishwa Wizara tofauti zinaainishwa kwa uwazi zaidi ili kuepusha mkanganyiko wakati wa uchambuzi wa bajeti. Aidha, Serikali ihakikishe kuwa taarifa za utekelezaji wa bajeti hizi zinatoa picha halisi ya uhusiano kati ya fedha zilizoidhinishwa, zilizohamishwa na zilizotekelezwa. Aidha, Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kuendelea kuimarisha uratibu wa taarifa za kibajeti kati ya programu na wizara zilizounganishwa ili kuongeza uwazi, ufanisi na urahisi wa ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma. Hatua hizi zitasaidia kuongeza ufanisi katika kuimarisha usimamizi bora wa bajeti za Serikali. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | kawaida kwa mujibu wa bajeti za programu zilizohamishiwa Wizara hii. | |
| 2 | Kwa Mwaka wa fedha 2026/2027 mfuko wa uwezeshaji umeidhinishiwa jumkla ya TZS 47,300,000,000 bilioni kwa ajili ya kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wananchi. Kwa kuwa mfuko huu unajumuisha fedha zinazozunguka (Revolving Fund), fedha hizo zilizoidhinishwa zimezingatiwa vipi kujumuishwa pamoja na fedha zinazorejeshwa kwenye mfuko jadi kipindi cha mwezi juni 2026. | Kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Mfuko wa Uwezeshaji umeidhinishiwa jumla ya TZS 47,300,000,000 kwa ajili ya kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wananchi. Fedha hizo ni za kuongeza mtaji katika Mfuko huo na hazijumuishi fedha za marejesho ya mikopo iliyotolewa hadi Juni, 2026. Kwa kawaida, fedha za marejesho ya mkopo huwa zinaendelea kutolewa mikopo kwa waombaji wengine ambao wako katika kusubiria mikopo mara tu baada ya kurejeshwa. Hii inaonekana katika ongezeko la waliopokea mikopo kutoka shabaha iliyowekwa. Mfano, kwa mwaka 2025/2026 matarajio ilikuwa ni kuwapatia mikopo wananchi 12,000 na uhalisia ni kuwa wananchi 30,000 walipatiowa mikopo. Ongezeko hilo linatokana na fedha zilizorejeshwa. | Kamati inaishauri Serikali kuimarisha zaidi mfumo wa usimamizi wa Mfuko huo kwa kuweka uwazi na ufuatiliaji wa karibu wa fedha za marejesho ili kuhakikisha zinarejeshwa kwa wakati na kutumika kwa ufanisi katika kutoa mikopo kwa walengwa wengi zaidi. Aidha, Serikali iandae taarifa za kina na za wazi zinazobainisha tofauti kati ya mtaji mpya na fedha zinazotokana na marejesho ili kurahisisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mfuko. Aidha, Kamati inasisitiza umuhimu wa kuimarisha mifumo ya kidijitali ya usimamizi wa mikopo ili kuongeza ufanisi, kupunguza ucheleweshaji wa marejesho na kupanua wigo wa wanufaika wa Mfuko huo. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3 | Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji itoe matarajio ya mfuko wa uwezeshaji (Likely outturn) kwa kipindi cha mwaka 2025/2026 ili kuweza kufahamu thamani ya mfuko ifikapo mwezi juni 2026. | Matarajio ya Mfuko wa Uwezeshaji (likely outrun) kwa kipindi cha mwaka 2025/2026 ni TZS 16,122,788,760.98 ambazo zitakuwa katika mzunguko (revolving). Hata hivyo, kiasi cha fedha kinachoratajiwa kuweza kutolewa mikopo ni TZS 8,120,320,710.20 kinachotokana na fedha za mzunguko kupitia mikopo iliyotolewa mwaka wa fedha 2025/2026. Hivyo, jumla ya fedha ambazo zinatarajiwa kutolewa mikopo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ni TZS 55,420,320,710.20 (TZS 47,300,000,000 + TZS 8,120,320,710.20) kwa wanufaika 33,210 (28,339 bajeti + 4871 revolving). | Kamati inaishauri Serikali kuimarisha mifumo ya upangaji na uwasilishaji wa taarifa za Mfuko kwa kuonesha kwa uwazi zaidi mtiririko wa fedha za bajeti (budget allocation) na fedha za mzunguko (revolving funds), ili kurahisisha ufanisi katika utekelezaji wa bajeti yake. Kamati inasisitiza umuhimu wa kufanya tathmini ya mara kwa mara ya ufanisi wa Mfuko huo kwa kuzingatia idadi ya wanufaika na thamani ya fedha zinazozunguka, ili kuhakikisha kuwa lengo la kuwawezesha wananchi kiuchumi linafikiwa kwa tija zaidi na kwa uwazi wa hali ya juu. |

## MAENEO AMBAYO YALICHANGIWA NA WAJUMBE WENGI

**Mheshimiwa Spika,** Wakati wa mijadala ya Bajeti za Wizara, Waheshimiwa Wajumbe walitoa michango mbalimbali kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Miongoni mwa michango hiyo, iligusa maeneo muhimu ambayo yalisisitizwa na Wajumbe wengi kutokana na umuhimu wake kwa maendeleo ya nchi na ustawi wa wananchi. Hivyo, kwa muhtasari, Kamati yangu inapenda kuyabainisha na kuyasisitiza maeneo hayo ili Serikali iyafanyie kazi kwa haraka na ufanisi, kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa Bajeti za Wizara na utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Maeneo hayo ni kama yafuatayo:

### Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais - Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi

**Mheshimiwa Spika,** Wakati wa mjadala wa bajeti ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Wajumbe wengi walisisitiza umuhimu wa kuimarisha uwezo wa nchi katika kukabiliana na maafa na kuitaka Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa kuwa na mipango madhubuti ya maandalizi na mwitikio wa haraka. Kamati inaunga mkono maoni hayo na kuishauri Kamisheni kuendelea kujiandaa kabla ya matukio ya maafa kutokea ili kupunguza madhara yanayoweza kujitokeza. Aidha, Kamati inasisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya Serikali, jamii, mashirika na sekta binafsi katika kukabiliana na maafa kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Suala la dawa za kulevya lilichangiwa kwa msisitizo mkubwa na Wajumbe wengi kutokana na athari zake kwa nguvu kazi na maendeleo ya nchi yetu. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha utoaji wa elimu kuhusu madhara ya dawa za kulevya, kuhamasisha ushiriki wa familia katika malezi na kinga, pamoja na kuendelea kuimarisha usimamizi wa sheria na udhibiti katika bandari, viwanja vya ndege na maeneo mengine ya kuingilia nchi katika nchi yetu, kwa lengo la kupunguza na hatimaye kutokomeza matumizi ya dawa hizo. Aidha, kwa kuwa, walioathirika na dawa za kulevya baada ya kupatiwa tiba hospitali huendelea kuzurura katika maeneo mbalimbali na kuleta taswira mbaya Kamati inaunga mkono ushauri wa kutafuta eneo lenye stara zaidi kwa utoaji wa huduma za tiba na uangalizi wa waathirika, ili kulinda maslahi ya jamii na makundi mengine hususan watoto.

**Mheshimiwa Spika,** Eneo jengine lililochangiwa na Wajumbe wengi katika Ofisi hii ni

suala la Tume ya Uchaguzi Zanzibar kuimarisha ufanisi katika mchakato mzima wa uchaguzi ili kuwawezesha wananchi kutumia haki yao ya kikatiba ya kuchagua viongozi wanaowataka katika mazingira ya amani na utulivu. Aidha, Wajumbe walisisitiza umuhimu wa kuimarishwa kwa elimu ya mpiga kura ili kuwawezesha wananchi kufahamu haki, wajibu na nafasi yao katika mchakato wa kidemokrasia. Kamati inaunga mkono maoni hayo na inaishauri Tume kuendelea kutoa elimu kwa umma kwa njia endelevu ili kuongeza uelewa na ushiriki wa wananchi katika uchaguzi. Vilevile, Kamati inasisitiza Tume kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa weledi, uwazi na haki, sambamba na kuyafanyia kazi kwa wakati malalamiko na maoni yanayotolewa na wadau mbalimbali wa uchaguzi, ikiwemo vyama vya siasa. Hatua hizi zitasaidia kuimarisha imani ya wananchi na kuimarisha zaidi usimamizi wa chaguzi zijazo.

**Mheshimiwa Spika,** Suala jengine ambalo Wajumbe wengi walilichangia kwa msisitizo ni kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), wakieleza kuwa umeendelea kuwawezesha wananchi kujikwamua na umaskini kupitia miradi mbalimbali ya kijamii. Hata hivyo, Wajumbe pia wamebainisha baadhi ya changamoto katika utekelezaji, ikiwemo tuhuma za uwepo wa upendeleo katika baadhi ya maeneo, jambo linalohitaji kufanyiwa ufuatiliaji na kuimarishwa. Kwa kuwa Mfuko huu unatekeleza miradi ya miundombinu na maendeleo katika maeneo maalum yaliyochaguliwa, Kamati inasisitiza umuhimu wa uwazi na usawa katika uteuzi wa walengwa pamoja na usimamizi wa miradi hiyo. Aidha, Kamati inatoa wito kwa wananchi kushiriki kikamilifu katika utekelezaji na ulinzi wa miradi inayotekelezwa katika maeneo yao ili kuongeza ushiriki wa jamii na kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa kwa ufanisi.

## Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ilipokea michango mingi kuhusu suala la uchimbaji wa kifusi, ambapo Waheshimiwa Wajumbe walieleza kuwa shughuli hiyo imeacha mashimo mengi yanayohatarisha usalama wa wananchi na kuathiri mazingira. Kamati inaunga mkono ushauri wa Wajumbe kwamba uchimbaji huo ufanywe kwa kitaalamu na maeneo husika yarudishwe katika hali yake ya awali ili kulinda mazingira na kupunguza hatari za maafa. Aidha, Kamati inaishauri Ofisi hii kufanya utafiti wa kina ili kuhakikisha rasilimali hiyo inatumika kwa njia

endelevu na salama kwa maslahi ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Suala la upatikanaji wa mikopo ya 4.4.2 kwa watu wenye mahitaji maalum ni miongoni mwa masuala yaliyowekewa msisitizo mkubwa na Wajumbe wakati wa mjadala wa bajeti ya Wizara hii. Wamebainisha kuwa utaratibu wa mikopo hiyo kupitia vikundi unaleta changamoto kwa watu wenye ulemavu kushiriki kikamilifu, hivyo kuwanyima fursa sawa ya kunufaika na mikopo hiyo. Kamati inaishauri Serikali kufanya mapitio ya vigezo vya utoaji wa mikopo hiyo ili kuzingatia hali halisi ya watu wenye ulemavu, ikiwemo kuanzisha utaratibu mbadala unaowawezesha kupata mikopo binafsi au kupitia vyama maalum vya walemavu. Aidha, Kamati inapendekeza kuimarishwa kwa elimu ya upatikanaji wa mikopo na kuweka mazingira wezeshi yatakayohakikisha usawa na ujumuishi katika fursa za kiuchumi kwa makundi yote.

**Mheshimiwa Spika,** Suala jengine ambalo Wajumbe walilichangia kwa msisitizo ni kuhusiana na upatikanaji mdogo wa fedha katika baadhi ya programu za Wizara hii. Wajumbe walibainisha changamoto ya mgao mdogo wa fedha hususan kwa Tume ya UKIMWI iliyopata asilimia 33 na ZEMA katika programu ya usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi iliyopata asilimia 18, hali inayoathiri utekelezaji wa majukumu yake muhimu. Waheshimiwa Wajumbe walishauri Serikali kuongeza mgao wa fedha katika maeneo hayo muhimu. Kamati inaunga mkono ushauri huo na kuisisitiza Serikali kuongeza mgao wa fedha katika Tume ya UKIMWI na ZEMA ili kuziwezesha taasisi hizo kutekeleza kikamilifu majukumu yao ya msingi, hususan katika mapambano dhidi ya UKIMWI, uhamasishaji wa jamii, na usimamizi endelevu wa mazingira pamoja na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Hatua hii itasaidia kuimarisha utekelezaji wa programu hizo muhimu na kufikia malengo ya kitaifa na kimataifa kwa ufanisi zaidi.

## Ofisi ya Rais - Ikulu

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuchangia Bajeti ya Ofisi ya Rais Ikulu, Waheshimiwa Wajumbe walielekeza msisitizo mkubwa kuhusu nafasi ya Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi (Diaspora) katika kuchangia maendeleo na kukuza uchumi wa Zanzibar kupitia uwekezaji na michango mbalimbali. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutambua mchango wao pamoja na kuweka mazingira rafiki kwa kupunguza urasimu na kurahisisha taratibu ili kuongeza ushiriki wao katika

maendeleo ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Eneo jengine ambalo Wajumbe wengi walichangia kwa msisitizo mkubwa mi kuhusu mafanikio ya mfumo wa Sema na Rais Mwinyi (SNR) ambao umeonekana kuleta tija kubwa katika kutoa maoni, kueleza changamoto, au kuwasilisha malalamiko moja kwa moja na kufuatilia hatua za utatuzi kwa wakati. Kamati inaishauri Serikali, kuongeza ufanisi katika utatuzi wa kero zinazowasilishwa kupitia mfumo huo ili kuhakikisha tija iliyokusudiwa inapatikana kikamilifu, sambamba na kuimarisha utaratibu wa kutoa mrejesho kwa wananchi walioleta kero zao ili kuongeza imani na ushiriki wao katika mfumo huo.

**Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ**

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuichangia Ofisi hii, suala la udhibiti hafifu wa taka na usafi wa mazingira limepewa msisitizo mkubwa na Wajumbe wengi, hususan katika maeneo ya Mji wa Zanzibar ikiwemo pembezoni mwa barabara, maeneo ya biashara na kuongezeka kwa utupaji holela wa taka katika maeneo ya makaazi, hali inayoonesha changamoto katika usimamizi duni wa mazingira. Kamati inaishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kuimarisha mifumo ya usimamizi wa usafi mijini ili kuhakikisha mazingira yanakuwa safi, salama na endelevu. Hii ni muhimu katika kuunga mkono dhamira ya kuifanya Zanzibar kuwa kitovu cha utalii Afrika, sambamba na kulinda afya na ustawi wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wengi pia wameeleza changamoto katika usimamizi wa maegesho ya gari katika maeneo mbalimbali ya Mji wa Zanzibar, ikiwemo kuwepo kwa baadhi ya watendaji wasio waaminifu wanaojipatia kipato nje ya utaratibu, pamoja na kuwepo udhaifu wa mifumo ya usimamizi wa maegesho unaosababisha malimbikizo ya madeni kwa madereva. Vilevile, kumekuwepo na muingiliano katika ukusanyaji wa mapato ya maegesho kati ya Mamlaka ya Mji Mkongwe na Manispaa ya Mjini. Kamati inaishauri, Serikali kusimamia vyema utaratibu mzima maegesho kwa kuyaimarisha zaidi ikiwa ni pamoja na kufuatilia kwa ukaribu kampuni zinazosimamia maegesho na utendaji kazi wa wafanyakazi wa maegesho. Aidha, Serikali itathmini upya mifumo inayotumika katika kukusanyia mapato na kuifanyia marekebisho inapohitajika ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato na bila ya kuwabambikizia madeni watumiaji wa maegesho hayo.

## Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora

**Mheshimiwa Spika,** Michango ya Waheshimiwa Wajumbe kuhusu Ofisi hii ilisisitiza umuhimu wa kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Maadili, huku pia ikiipongeza kwa ufanisi wake katika kusimamia wajibu wake. Kwa mujibu wa Sheria, Tume hii ina jukumu la kusambaza fomu zinazopaswa kujazwa na viongozi wote wa umma waliotajwa katika sheria hiyo ndani ya muda uliowekwa. Kutokana na changamoto za muda na uhitaji wa kuwasilisha fomu hizo kwa wakati, Wajumbe wengi walipendekeza kuwepo kwa mfumo wa kielektroniki wa ujazaji na uwasilishaji wa fomu hizo ili kurahisisha mchakato, hususan kwa viongozi wanaoweza kuwa nje ya nchi wakati wa zoezi hilo. Kamati inaunga mkono pendekezo hilo kwa kuwa litaimarisha ufanisi, uwazi na uwasilishaji wa fomu kwa wakati unaotakiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kupitia Ofisi ya Kadhi, Wajumbe wengi walisisitiza umuhimu wa kushughulikia kwa umakini masuala ya ndoa na talaka kutokana na ongezeko la migogoro inayowasilishwa katika Ofisi hiyo. Kamati inaishauri Ofisi ya Kadhi kuhakikisha usikilizaji wa mashauri unahusisha pande zote mbili ili kutoa fursa ya kusikilizwa kwa haki na kufikia maamuzi ya haki na yenye uadilifu. Aidha, Kamati inatoa wito kwa jamii kuimarisha elimu ya ndoa ili kupunguza migogoro, kuimarisha familia na kuchangia malezi bora ambayo ni msingi wa maendeleo ya taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wengi pia walisisitiza suala la kuimarisha maslahi ya walimu wa madrasa na kuiomba Serikali kupitia Ofisi ya Mufti kuwapa msaada kutokana na hali ya umasikini inayoathiri wengi wao. Kwa kuzingatia wigo mpana wa walimu hao na uwezo mdogo wa Ofisi kulipa posho kwa wote, Kamati inaishauri Ofisi ya Mufti kuendelea kutafuta wadhamini na washirika wa maendeleo ili kuwasaidia walimu hao, sambamba na kuhamasisha jamii kulipa ada za madrasa kwa wakati ili kusaidia uendeshaji endelevu wa huduma hizo. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kulitafutia ufumbuzi wa kudumu suala hili kutokana na umuhimu mkubwa wa walimu wa madrasa katika malezi ya kimaadili ya watoto wetu, kwani mchango wao ni msingi katika kujenga jamii yenye maadili mema, kuwa raia wema na kupunguza vitendo vya kihalifu na mmomonyoko wa maadili.

## Wizara ya Kazi na Uwekezaji

**Mheshimiwa Spika,** Katika mjadala wa Wizara ya Kazi na Uwekezaji, Wajumbe wengi

walisisitiza suala la upatikanaji wa ajira kwa wazawa katika fursa mbalimbali zilizopo nchini. Wamebainisha kuwa licha ya uwepo wa miradi mikubwa ya maendeleo hususan ya ujenzi na katika sekta ya utalii, bado hawanufaiki ipasavyo na ajira zinazozalishwa, ambapo katika baadhi ya maeneo wageni wamekuwa wakipata fursa zaidi za ajira kuliko wazawa. Hali hii imeibua wasiwasi wa Wajumbe kuhusu usawa na uwiano wa manufaa ya kiuchumi kwa wananchi. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha sera na mikakati ya upendeleo wa kipaumbele kwa wazawa katika ajira, ikiwemo kuweka utaratibu wa uwiano wa ajira katika miradi yote na katika hoteli za kitalii pamoja na kuimarisha ujuzi kwa wazawa ili waweze kushindana kikamilifu katika soko la ajira. Hatua hii itahakikisha wazawa wanakuwa wanufaika wakuu wa rasilimali na fursa za kiuchumi zinazozalishwa nchini.

### Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wengi wakati walipokuwa wakichangia bajeti ya Wizara hii, walionesha kuguswa na kuwepo kwa changamoto ya upungufu wa walimu katika skuli za msingi na sekondari, hali inayoathiri kwa kiasi kikubwa ubora wa ufundishaji na kujifunza kwa wanafunzi. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha mpango wa ajira za walimu na kufanya mgawanyo kwa uwiano sahihi ili kupunguza pengo lililopo na kuinua ubora wa elimu katika ngazi zote za skuli za msingi na sekondari.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo jengine ambalo limesisitizwa na Wajumbe ni umuhimu wa kuimarisha mitaala ya elimu ya amali ili iendane na mabadiliko ya dunia ya sasa na mahitaji ya soko la ajira. Ili kufanikisha lengo hilo, ni lazima Serikali ihakikishe inajipanga kikamilifu katika kuweka mazingira wezeshi yakiwemo upatikanaji wa vifaa vya mafunzo, wataalamu wenye weledi, vitendea kazi vya kutosha pamoja na miundombinu bora. Kamati inaishauri Serikali, kuendelea kuimarisha sekta ya elimu ya amali kwa kuimarisha mitaala ili kuendana na mahitaji ya sasa, sambamba na kuwawezesha wahitimu wa fani za amali kwa kuwapatiwa vifaa vya kazi na fursa za mitaji ili waweze kujiajiri na kuanzisha shughuli za uzalishaji badala ya kusubiri kuajiriwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine katika Wizara hii, Wajumbe wengi waliweka msisitizo kuhusu kuwepo kwa changamoto ya uchelewaji wa mikopo ya elimu ya juu inayotolewa na Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu, hali

inayowaathiri wanafunzi katika kuendelea na masomo yao na utekelezaji wa mipango yao ya kielimu na maisha ya chuoni. Wajumbe wameeleza kuwa upatikanaji wa mikopo hiyo kwa wakati ni muhimu ili kuwawezesha wanafunzi kuendelea na masomo bila kukwama na kupunguza changamoto za kifedha zinazowakabili. Kamati inaishauri Serikali, kuendelea kujipanga kifedha kwa kuhakikisha inaongeza mgao wa fedha kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu ili kukidhi mahitaji halisi ya wanafunzi na kuhakikisha mikopo hiyo inatolewa kwa wakati bila kuchelewa, hivyo kuwawezesha wanafunzi kuendelea na masomo yao kwa utulivu na kufanikisha malengo yao ya kitaaluma.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo**

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe kuhusu Wizara hii ni suala la uhifadhi wa misitu ya jamii kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa za misitu kama dawa za asili. Kamati inaunga mkono hoja hiyo na inaishauri Wizara kuimarisha ulinzi wa misitu ya hifadhi ya jamii kwa kushirikiana na vikundi vya Shehia, kuweka mipaka na ulinzi madhubuti ili kudhibiti ukataji holela wa miti, pamoja na kuongeza juhudi za upandaji wa miti hususan ya dawa za asili inayotoweka kwa kasi. Sambamba na hilo, Serikali inapaswa kuimarisha utekelezaji wa mikakati ya upatikanaji wa nishati mbadala ya kupikia, ikiwemo gesi na umeme, ili kupunguza utegemezi wa kuni na makaa. Bila hatua hiyo, juhudi za kuzuia ukataji miti kwa ajili ya kuni na makaa zitakuwa na changamoto kubwa katika kufanikiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine katika Wizara hii, Wajumbe wengi walisisitiza umuhimu wa mageuzi katika Sekta ya Kilimo ili kuendana na kilimo cha kisasa kinachotumia teknolojia ya kisasa, katika umwagiliaji, matumizi bora ya pembejeo, pamoja na kupatikana wataalamu wenye weledi katika kilimo cha kisasa. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha marekebisho ya sekta hiyo ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, kupunguza utegemezi wa bidhaa za chakula kutoka nje, na hatimaye kuinua kipato cha wananchi pamoja na kupunguza gharama za maisha kupitia upatikanaji wa chakula kwa bei nafuu.

**Wizara ya Afya**

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wengi wakati walipokuwa wakichangia bajeti ya Wizara ya Afya, walionesha kuguswa na kusisitiza umuhimu wa ujenzi na

ukamilishaji wa vituo vya afya katika maeneo yao, huku baadhi wakiiomba Serikali kuvijenga upya vituo vilivyochakaa ili kuimarisha utoaji wa huduma za afya. Vilevile, suala la upungufu wa nyumba za madaktari lilijadiliwa kwa kina, ambapo Wajumbe walishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuhakikisha zinajengwa ili kuwawezesha watumishi wa afya kuishi karibu na vituo vyao na kutoa huduma kwa ufanisi, ikiwemo za dharura. Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Afya kwa juhudi inazozichukua katika kuimarisha miundombinu ya afya, na inaishauri kuendelea kufuatilia kwa karibu pamoja na kufanya ukarabati au ujenzi upya wa vituo ambavyo haviko katika viwango stahiki ili kuimarisha zaidi huduma kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Suala la upatikanaji wa dawa na vifaa tiba pia limechangiwa na Wajumbe wengi katika Wizara hii, wakibainisha kuwepo kwa uhaba katika baadhi ya hospitali na vituo vya afya hali inayosababisha wananchi kukosa baadhi ya huduma muhimu za tiba. Kamati inaitaka Serikali kuendelea kuimarisha usambazaji wa dawa na kufuatilia kwa karibu maeneo yenye upungufu, sambamba na kuwasisitiza wasimamizi wa vituo vya afya kufuata taratibu za uagizaji na usimamizi wa dawa ili kuondoa changamoto hiyo. Kwa ujumla, Kamati inaamini kuwa ufuatiliaji madhubuti utaimarisha upatikanaji wa dawa na kuimarisha huduma za afya kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Suala la kuimarishwa maslahi ya watendaji wa sekta ya afya nalo limepewa uzito na Wajumbe ambapo walisisitiza mchango mkubwa wa watendaji hao katika utoaji wa huduma kwa wagonjwa katika hospitali na vituo vya afya, wakiwemo watendaji wote kuanzia wahudumu wa kawaida hadi madaktari bingwa, hivyo maslahi yao yanapaswa kuimarishwa ili kuongeza ufanisi wa huduma. Kamati inaunga mkono maoni hayo ya Wajumbe kwani hatua hiyo itaongeza motisha, uadilifu na ari ya kazi, kupunguza uhamaji wa wataalamu, na hatimaye kuimarisha huduma za afya na kuokoa maisha ya wananchi kwa manufaa ya maendeleo ya nchi.

## Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda

**Mheshimiwa Spika,** Katika Wizara hii, ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, suala la ukuzaji wa viwanda limepewa msisitizo mkubwa na Wajumbe wengi, wakibainisha kudorora kwa baadhi ya viwanda vya ndani kama BASRA na Kiwanda cha Maziwa cha Bakhresa Fumba, hali inayopunguza uwezo wa uzalishaji wa ndani na kuathiri kasi ya ukuaji wa uchumi wa Zanzibar. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi za kufufua, kuimarisha na kulinda viwanda vya ndani kwa kubaini na

kushughulikia vikwazo vinavyosababisha kudorora kwake, ikiwemo gharama za uzalishaji, mazingira ya uwekezaji na usimamizi. Hatua hizi zitachochea uzalishaji wa ndani, kuongeza ajira na kuimarisha uchumi wa nchi yetu kwa ujumla.

## Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale

**Mheshimiwa Spika,** Katika mjadala wa Wizara hii, Wajumbe wengi walichangia suala la utoaji wa vibali vya ujenzi ndani ya Mji Mkongwe, ambapo kumekuwepo na malalamiko kuhusu ucheleweshaji na ugumu wa upatikanaji wa vibali kwa wananchi wanaokusudia kuendeleza majengo yao kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa. Wajumbe walieleza kuwa hali hiyo imekuwa ikikwamisha baadhi ya shughuli za maendeleo na uwekezaji katika eneo hilo. Aidha, Wajumbe walisisitiza umuhimu wa kuwepo kwa uwiano mzuri kati ya uhifadhi wa Mji Mkongwe kama urithi wa kihistoria na kitamaduni na mahitaji ya maendeleo ya wananchi. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha mifumo ya uratibu na utoaji wa vibali kwa kuongeza uwazi na ufanisi, sambamba na kuhakikisha shughuli za uhifadhi na uendelezaji wa Mji Mkongwe zinatekelezwa kwa kuzingatia sheria na maslahi ya wananchi pamoja na hifadhi ya urithi wa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Suala la jengine lililochangiwa kwa msisitizo mkubwa na Wajumbe ni kuimarishwa kwa fursa za kiuchumi kwa vijana wa Zanzibar kupitia sekta ya utalii jumuishi, ikizingatiwa kuwa sekta hiyo inachangia zaidi ya asilimia 30 ya Pato la Taifa. Wajumbe wameeleza haja ya kuhakikisha wazawa wananufaika ipasavyo na fursa zilizopo katika sekta hiyo kupitia ajira, ujasiriamali na ushiriki mpana katika mnyororo wa thamani wa utalii, sambamba na kurejesha nidhamu katika sekta hususan katika huduma za waongoza watalii (tour guides) na ushiriki wa kampuni za nje ili kulinda na kuwezesha fursa hizo kubaki kwa wananchi wa Zanzibar. Aidha, Wajumbe walisisitiza umuhimu wa kuendeleza utalii endelevu (sustainable tourism) kwa kuhakikisha ukuaji wa sekta hiyo unaenda sambamba na uhifadhi wa mazingira na maliasili za visiwa vyetu. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha usimamizi wa sekta ya utalii ili kuhakikisha inawanufaisha zaidi wazawa na wakati huohuo inalinda mazingira kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

## Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

**Mheshimiwa Spika,** Katika mjadala wa Wizara hii walieleza kuridhishwa na hatua za

Serikali katika kuwatunza wazee, hususan utoaji wa pensheni ya jamii kwa waliofikia umri wa miaka sabini na uimarishaji wa makazi ya wazee Sebleni Unguja na Limbani Pemba. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwathamini na kuwatunza wazee wetu waliolitumikia taifa, sambamba na kuishauri Wizara kuendelea kuimarisha makaazi ya wazee kwa kuweka huduma muhimu ikiwemo viwanja vya mazoezi, pamoja na kuhakikisha usajili wa wazee wote wanaostahiki pensheni ya jamii unafanyika kwa wakati, haki na bila ubaguzi wa aina yoyote.

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wengi pia walisisitiza umuhimu wa kuimarisha uwezeshaji wa wajasiriamali, hususan vikundi vya wanawake, kupitia upatikanaji wa mikopo ili kuwawezesha kuinuka kiuchumi. Kamati inaishauri Wizara kuimarisha usimamizi wa programu za uwezeshaji kwa kuhakikisha vikundi vya wanawake wajasiriamali vinapatiwa mikopo nafuu na kwa wakati ili kuendeleza shughuli zao za uzalishaji na kuchochea maendeleo ya kiuchumi.

**Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu**

**Mheshimiwa Spika,** Michango mingi ya Waheshimiwa Wajumbe katika Wizara hii ilijikita katika suala la ushirikiano na kusomana kwa mifumo ya Serikali jambo ambalo limepewa msisitizo na Wajumbe wengi kutokana na umuhimu wake katika kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya umma na utoaji wa huduma kwa wananchi. Wajumbe wamebainisha kuwa mifumo hiyo inaposoma hurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wakati, hupunguza urudufu wa kazi, huongeza uwazi na kuimarisha kasi ya utoaji wa huduma za Serikali. Kamati inaishauri Wizara kuimarisha zaidi uunganishaji na ushirikiano wa mifumo hiyo sambamba na kuweka miundombinu madhubuti ya usalama wa mtandao ili kulinda taarifa za Serikali dhidi ya uvujaji, udukuzi na matumizi yasiyo sahihi. Hatua hiyo itachochea ufanisi, uwajibikaji na kuimarisha imani ya wananchi katika utoaji wa huduma za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Eneo jengine ambalo lilichangiwa na Wajumbe wengi ni kuwepo kwa changamoto ya upatikanaji wa mtandao usio thabiti, hususan katika vifurushi vya simu ambapo gharama hukatwa bila huduma kuwa na ubora unaotarajiwa, hali inayosababisha usumbufu kwa watumiaji na kuathiri upatikanaji wa huduma. Kamati inaitaka Serikali, kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano ya Tanzania Bara na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kufuatilia kwa karibu utendaji wa watoa

huduma za mawasiliano ili kuhakikisha wanazingatia viwango vya ubora vinavyolingana na gharama zinazolipwa na wananchi. Aidha, Kamati inashauri kufanyika kwa mapitio ya gharama za vifurushi vya huduma za mtandao ili ziwe nafuu, zenye uwiano na ubora wa huduma inayotolewa, hatua itakayosaidia kuimarisha ufanisi, uaminifu na upatikanaji bora wa huduma za mawasiliano kwa wananchi.

### Wizara ya Maji, Nishati na Madini

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wengi walitumia muda wao katika mjadala wa Wizara hii kuisisitiza Serikali kuhusu changamoto ya upatikanaji wa maji katika maeneo mengi ya Zanzibar, licha ya juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali kuimarisha huduma hiyo. Wajumbe wameibua hoja kuhusu matumizi ya matangi makubwa ya kuhifadhia maji, ambapo muda mrefu hutumika kuyajaza ilhali maji hayo hutumika kwa muda mfupi kabla ya kuisha, hali inayochangia upungufu wa huduma katika maeneo mengi. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Maji kuandaa na kutekeleza mkakati wa muda mfupi na mrefu ikiwemo kuimarisha miundombinu ya usambazaji, kuongeza uwezo wa uzalishaji wa maji, kupunguza upotevu wa maji katika mfumo (leakages), pamoja na kuimarisha usimamizi wa matengenezo ya mara kwa mara. Hatua hizi zitasaidia kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi na ya uhakika kwa ufanisi na uendelevu zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Suala jengine lililojadiliwa sana katika Wizara hii ni kuhusu suala la upatikanaji wa umeme wa uhakika Zanzibar kutokana na athari zake katika uwekezaji, biashara na ustawi wa uchumi kwa ujumla. Pamoja na Serikali kuanza kutekeleza mikakati ya muda wa kati na mrefu ya kuimarisha huduma hiyo, Kamati inaishauri Wizara kuharakisha utekelezaji wa mikakati ya muda mfupi ikiwemo kuimarisha matengenezo ya miundombinu ya umeme, kuongeza ufuatiliaji wa mara kwa mara wa hitilafu, na kuimarisha mfumo wa majibu ya haraka pindi panapotokea hitilafu. Aidha, Serikali iendelee kuwekeza katika vyanzo mbadala na imara vya umeme ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya uhakika na endelevu kwa wananchi na sekta ya uzalishaji.

### Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi

**Mheshimiwa Spika,** Waheshimiwa Wajumbe katika michango yao kuhusu bajeti ya

Wizara hii, walisisitiza umuhimu wa kuimarisha kilimo cha mwani pamoja na masoko yake, ikizingatiwa kuwa mwani ni zao la kimkakati linalowezesha wananchi wetu, hususan wanawake, kupata kipato na kuchangia katika ustawi wa familia zao na pato la taifa kwa ujumla. Wajumbe wameeleza kuwa licha ya mchango wake mkubwa, bado sekta hiyo inakabiliwa na changamoto ya bei kutokuwa ya uhakika na kuuza bidhaa ikiwa katika hali ya ghafi, jambo linalopunguza tija na manufaa kwa wazalishaji. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha mfumo wa masoko ya mwani pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa bei yenye tija na ya uhakika kwa wakulima, sambamba na kuharakisha uanzishaji na uendeshaji wa kiwanda cha mwani ili kuongeza thamani ya zao hilo na kuinua kipato cha wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo jengine ambalo limesisitizwa na Wajumbe ni suala la umuhimu wa maendeleo ya sekta ya mafuta na gesi asilia, hususan hatua zinazochukuliwa za utafiti kupitia 2D na 3D Seismic Survey ambazo kwa sasa zinaendelea ili kubaini uwepo wa rasilimali hizo katika maeneo husika. Wajumbe wameeleza umuhimu wa Serikali kuharakisha kukamilisha tafiti hizo ili kupata majibu ya uhakika kuhusu uwepo wa mafuta na gesi asilia na kuanza hatua za uwekezaji. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha mchakato wa utafiti na maandalizi ya sekta hiyo, na pale matokeo yatakapothibitisha uwepo wa rasilimali hizo, Serikali iwe na maandalizi ya kutosha ya kuanza uchimbaji wa visima vya mafuta na gesi asilia ifikapo mwaka 2028 ili kuhakikisha Taifa linanufaika na rasilimali zake za kimkakati.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine katika Wizara hii, Wajumbe wengi wakati walipokuwa wakichangia bajeti ya Wizara hii, walionesha kuguswa na hali ya utendaji na ufanisi wa baadhi ya taasisi za umma, hususan ZAFICO, ambapo wameeleza kutoridhishwa na kiwango cha tija inayotokana na uwekezaji wa fedha za walipakodi katika taasisi hiyo. Wajumbe wameeleza kuwa kuna haja ya kufanya tathmini ya kina ya utendaji wake ili kubaini kama inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuleta manufaa yanayotarajiwa kwa wananchi na Taifa kwa ujumla, badala ya kujikita zaidi katika shughuli za kibiashara zinazofanana na zile za wananchi wa kawaida bila kuongeza thamani katika sekta ya uvuvi. Kamati inaishauri Serikali kufanya mapitio ya kina ya taasisi hiyo na nyingine zenye changamoto za kiutendaji, na pale itakapobainika kutokidhi malengo yake ya msingi, kuchukua hatua stahiki ikiwemo kuimarisha au kuboresha upya muundo wake ili kuhakikisha sekta ya uvuvi

inachochewa kwa weledi, tija na uendelevu kwa kuwa nchi imebarikiwa rasilimali na wataalamu wa kutosha katika sekta hiyo.

### Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi

**Mheshimiwa Spika,** Katika mjadala wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, wameipongeza Serikali kwa jitihada za kuimarisha miundombinu ya barabara mijini na vijijini Unguja na Pemba, hata hivyo wamesisitiza umuhimu wa kuendelea na ukarabati na ujenzi wa barabara ambazo bado hazijafanyiwa matengenezo katika maeneo mengine ili kurahisisha huduma za usafiri kwa wananchi. Kamati inaishauri Wizara kuendelea kuimarisha miundombinu ya barabara kwa kuzingatia viwango vya ubora na upana unaostahiki ili kuongeza usalama na kupunguza msongamano wa magari. Aidha, Serikali ihakikishe inawapatia zabuni wakandarasi wenye weledi, uwezo na uzoefu ili kujenga barabara imara na zitakazoweza kudumu kwa muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika,** Eneo jengine lililochangiwa na Wajumbe wengi tena kwa msisitizo mkubwa ni kuwepo kwa malalamiko mengi ya wananchi wanaopisha miradi ya maendeleo. Kamati inaisisitiza Serikali kuendelea kusimamia kwa umakini na uwazi mchakato wa ulipaji wa fidia, kwani bado kuna wananchi katika maeneo mbalimbali ambao hawajapatiwa haki zao kwa wakati hali inayowarudisha nyuma sana kiuchumi. Aidha, kumekuwepo na malalamiko kuwa baadhi ya fidia zinazolipwa hazilingani na thamani halisi ya maeneo na mazao yaliyopo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuimarisha mchakato wa uthamini wa fidia kwa kuhakikisha unafanyika kwa weledi, uwazi na ushirikishwaji wa wataalamu waliobobea pamoja na uwakilishi wa wananchi husika. Aidha, viwango vya fidia vizingatie thamani halisi ya maeneo na mazao ili kuhakikisha wananchi wanalipwa fidia stahiki na kwa haki, hatua itakayosaidia kuongeza imani na kupunguza malalamiko katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Vilevile, Serikali ipunguze kutumia muda mrefu katika mchakato wa uthamini na malipo ya fidia ili kuharakisha upatikanaji wa haki za wananchi kwa wakati na kuepusha matapeli na watendaji wasio waaminifu kujipenyeza katika mchakato wa malipo ya fidia.

### Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi

**Mheshimiwa Spika,** Michango ya Wajumbe wengi katika Wizara hii ilisisitiza suala la

kuwepo kwa changamoto ya migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikiathiri wananchi na kurudisha nyuma maendeleo yao. Kwa kuzingatia umuhimu wa ardhi kama rasilimali ya msingi ya maendeleo ya mtu mmoja mmoja na nchi kwa ujumla, Kamati inaona kuwa upatikanaji wa hati milki ni nyenzo muhimu ya kupunguza migogoro hiyo. Hata hivyo, Wajumbe pia wamebainisha kuwa kuwepo kwa utaratibu mrefu na mgumu wa upatikanaji wa hati ni miongoni mwa sababu zinazochangia kuendelea kuongezeka kwa migogoro hiyo. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Ardhi kurahisisha na kufupisha taratibu za upatikanaji wa hati milki ili kuongeza kasi ya urasimishaji wa maeneo. Vilevile, Serikali iandae mikakati ya kupima na kupangilia ardhi yote nchini ili kuhakikisha kila eneo linatambuliwa rasmi.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hilo, Kamati inaishauri Serikali kuweka urahisi zaidi katika taratibu za uhaulishaji wa ardhi pale wananchi wanapouziana maeneo yao, ili kuepusha mianya ya migogoro na kuhakikisha taarifa za umiliki zinabaki sahihi na zinaendana na taarifa kwa wakati huo. Hatua hizi kwa ujumla zitasaidia kupunguza migogoro ya ardhi, kuongeza usalama wa umiliki na kuchochea maendeleo ya kiuchumi kwa wananchi na pia kuongeza mapato ya Serikali.

## Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo

**Mheshimiwa Spika**, Katika mjadala wa Wizara hii Waheshimiwa Wajumbe walielekeza michango yao suala la ushiriki wa Zanzibar katika Shirikisho la Soka Afrika (CAF) ambapo Wajumbe walitaka kupatiwa ufafanuzi kuhusu sababu za Zanzibar kuondolewa uanachama na hatua zinazochukuliwa kuirejesha. Kamati inaishauri Wizara kulifuatilia kwa karibu na kwa uharaka suala hili kwa kushirikiana na mamlaka husika za kitaifa na kimataifa ili kuhakikisha Zanzibar inarejeshewa hadhi yake katika michezo ya kimataifa. Hatua hiyo itaimarisha ushiriki wa wanamichezo wetu, kuinua vipaji na kulinda heshima ya Zanzibar katika medani za michezo ya kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo jengine ambalo limesisitizwa na Wajumbe wengi ni suala la matumizi ya viwanja vipya vya michezo bila malipo limeibuliwa kwa msisitizo na Wajumbe wengi, hususan viwanja vinavyotumika katika ngazi za chini za ligi kwa ajili ya kuendeleza na kuibua vipaji vya watoto na vijana. Wajumbe wamebainisha kuwa kabla ya ujenzi wa viwanja hivyo, maeneo hayo yalikuwa yakitumika kwa mazoezi ya

kila siku na mashindano ya ligi, hali iliyosaidia kujenga afya ya vijana na kutoa wachezaji wengi wenye vipaji wanaocheza katika ligi kubwa ndani na nje ya nchi. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara hii kufanya tathmini ya matumizi ya viwanja hivyo na kuweka utaratibu maalum utakaohakikisha watoto na vijana wanaendelea kuvitumia kwa urahisi na bila vikwazo visivyo vya lazima. Hatua hii itaimarisha maendeleo ya michezo, kukuza vipaji vipya na kuendeleza mafanikio ya sekta ya michezo nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine katika Wizara hii, Waheshimiwa Wajumbe waligusia suala la kupungua kwa utamaduni wa Mzanzibari katika mavazi, hususan kutokana na mabadiliko ya mwenendo wa mavazi kwa wageni na baadhi ya wazawa. Wajumbe wengi wamesisitiza umuhimu wa kuwepo kwa sheria madhubuti pamoja na usimamizi wake ili kulinda mila, silka na utamaduni wa Mzanzibari. Kamati inaishauri Wizara kuandaa na kutekeleza mikakati mahsusi ya kuuenzi na kuulinda utamaduni wa Zanzibar, ikiwemo uhamasishaji wa jamii, elimu kwa umma na ufuatiliaji wa karibu wa utekelezaji wa kanuni zinazolinda maadili ya kitamaduni, ili kuhakikisha tunadumisha na kurithisha utambulisho wetu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

## Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji

**Mheshimiwa Spika,** Michango ya Waheshimiwa Wajumbe kuhusu Wizara hii ilisisitiza suala la kuwepo kwa changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana, hali inayochangiwa na upungufu wa fursa za kazi pamoja na ujuzi unaoendana na mahitaji ya soko la ajira. Wajumbe wameeleza umuhimu wa Serikali kuimarisha programu za kuwajengea vijana ujuzi wa vitendo, kuongeza uwezo wa kujiamini na kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Vijana ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi, hususan katika fursa za kazi zenye staha (decent jobs). Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha mipango ya uwezeshaji vijana kwa kutoa mafunzo ya stadi za kazi, kuendeleza ujasiriamali na kuweka mazingira wezeshi ya ajira, ili kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira na kuongeza ushiriki wa vijana katika maendeleo ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wengi wakati walipokuwa wakichangia bajeti ya Wizara hii, walionesha kuguswa na umuhimu wa kuimarisha mikopo ya uwezeshaji

kwa wananchi, hususan mikopo midogo midogo inayolenga kuwawezesha wajasiriamali, wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Wajumbe wameeleza kuwa bado kuna changamoto ya baadhi ya wanufaika kukosa ujuzi wa kutosha wa ujasiriamali na usimamizi wa biashara, jambo linalopunguza tija ya mikopo hiyo, pamoja na kuwepo kwa mzigo wa gharama ikiwemo kodi unaoathiri ukuaji wa biashara changa. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha programu za kuwajengea uwezo wajasiriamali kabla na baada ya kupatiwa mikopo, kuweka mazingira ya ahueni ya kodi kwa kipindi maalum kwa biashara changa, na kuhakikisha makundi maalum ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu yanapewa kipaumbele katika upatikanaji wa mikopo na fursa za kiuchumi ili kuongeza ushiriki wao katika maendeleo ya nchi yetu.

## Wizara ya Fedha na Mipango

**Mheshimiwa Spika,** Wakati wa mjadala wa Wizara ya Fedha na Mipango Wajumbe wengi wamezipongeza Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya katika ukusanyaji wa mapato. Hata hivyo, Wajumbe wamebainisha kuwepo kwa changamoto mbalimbali zinazohitaji kupatiwa ufumbuzi, ikiwemo baadhi ya wafanyabiashara kutotoa risiti za mauzo, wananchi kutodai risiti wanaponunua bidhaa na huduma, pamoja na malalamiko ya ulipaji wa kodi mara mbili kwa baadhi ya bidhaa zinazosafirishwa kati ya Zanzibar na Tanzania Bara. Kamati inaishauri Wizara kufuatilia kwa karibu changamoto hizo ili kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato na kuimarisha mazingira ya biashara. Aidha, juhudi zaidi zielekezwe katika kuhamasisha wananchi kudai risiti na kuimarisha usimamizi kwa wafanyabiashara wanaokiuka taratibu za utoaji wa risiti, kwani hali hiyo husababisha Serikali kukosa mapato stahiki na kufanya makadirio ya kodi yasiyoakisi hali halisi ya biashara zinazofanyika nchini.

**Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika,** Eneo jengine ambalo lilichangiwa na Wajumbe wengi ni suala la utegemezi wa bajeti ya Serikali pamoja na usimamizi wa bajeti kupitia Wizara ya Fedha na Mipango. Serikali imebainisha kuwa inaendelea kupunguza utegemezi huo kwa kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kutumia vyanzo vya ndani vya mikopo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, badala ya kutegemea kwa kiasi kikubwa misaada na ruzuku za washirika wa maendeleo. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuwa wakati wa kufanya

marekebisho ya sheria za kodi, ada na tozo mbalimbali, izingatie hali halisi ya uchumi na maisha ya wananchi wa Zanzibar. Hii ni kutokana na kuwepo kwa baadhi ya malalamiko kuhusu ongezeko la tozo, ada na faini ambazo hazilingani na uwezo wa wananchi. Kwa ujumla, hatua hizi zitasaidia kuimarisha uhimilivu wa wananchi katika ulipaji kodi, kuongeza mapato ya Serikali kwa uendelevu na kuhakikisha sera za kifedha zinazingatia hali halisi ya kiuchumi ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Suala la ufanisi katika utendaji kazi wa mashirika ya umma limejadiliwa kwa msisitizo mkubwa na Wajumbe wengi, ambao wameeleza wasiwasi wao kuhusu baadhi ya mashirika kushindwa kujiendesha kwa ufanisi na kibiashara, kushindwa kutoa huduma bora na kuchangia mapato ya Serikali kupitia gawio. Badala yake, baadhi ya mashirika yameendelea kutegemea ruzuku za Serikali ili kujiendesha, hali inayoongeza mzigo kwa Serikali. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha tathmini ya kina ya utendaji wa mashirika ya umma ili kubaini yale yenye uwezo wa kujiendesha na yale yasiyo na tija kwa uchumi wa nchi yetu. Aidha, Kamati inasisitiza mashirika hayo yawezeshwe kufanya kazi kwa misingi ya kibiashara, kwa kuyapa uhuru unaohitajika katika uendeshaji wake huku yakizingatia sheria, kanuni na miongozo iliyowekwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Katika hili mashirika ya umma, Kamati inaona kuwa jukumu kuu la Serikali linapaswa kuwa ni kusimamia utekelezaji wa sera, sheria na viwango vya utendaji, pamoja na kuhakikisha mashirika yanafanya kazi kwa ufanisi, uwazi na faida. Serikali iepuke kuyaendesha mashirika hayo kama idara za Wizara, kwani hali hiyo hupunguza ubunifu, ushindani na uwezo wa kufanya maamuzi ya kibiashara kwa wakati. Mashirika yanapopewa mazingira bora ya kujiendesha kwa tija, yataongeza mapato, kutoa huduma bora zaidi, kuchangia ukuaji wa uchumi na hatimaye kuipatia Serikali gawio badala ya kuendelea kutegemea ruzuku kutoka kwenye fedha za umma.

## HOJA ZA JUMLA

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kupitia upya mgawanyo wa rasilimali fedha kwa mafungu ya kibajeti mapya na ya zamani kwa mwaka wa fedha 2025/2026 yanayotokana na mabadiliko ya muundo wa Serikali.

Lengo la kupitia upya ni kutokana na utofauti uliojitokeza wa uwasilishaji wa taarifa za utekelezaji Kiwizara, tofauti na taarifa za Serikali kuhusu jambo hili zilizowasilishwa na kuidhinishwa na Baraza. Serikali ihakikishe mgawanyo wa fedha kufuatia uhamishaji wa mafungu hauathiri kiwango cha jumla cha fungu la bajeti kilichoidhinishwa na Kamati ya Matumizi ya Baraza.

**Mheshimiwa Spika,** Kumekuwepo na changamoto katika Mfumo wa Bajeti na Matumizi Serikalini (BAMAS), ambapo watendaji wamekuwa wakitumia muda mrefu kuingiza taarifa za bajeti za wizara na taasisi zao kutokana na kuwepo kwa mapungufu mbalimbali ya kiufundi katika mfumo huo. Ili kukabiliana na changamoto hii, Kamati inaishauri Serikali kuzingatia mojawapo ya njia mbili za utengenezaji wa mifumo ya TEHAMA. Kwanza, Wizara inaweza kuunda timu ya wataalamu wake wa TEHAMA ambao watahusika moja kwa moja katika kubuni na kutengeneza mfumo huo, na pale ambapo kutajitokeza mapungufu ya kitaalamu wapatiwe msaada kutoka kwa wataalamu wa nje kwa ajili ya mafunzo na ushauri wa kitaalamu. Mfano wa mbinu hii umetumika na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika utengenezaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Manunuzi ya Umma (NeST). Pili, Serikali inaweza kumuajiri mtaalamu au kampuni ya kitaalamu kutengeneza mfumo kwa mkataba maalum, ambapo msimbo msingi wa programu (source codes) zitabaki kuwa mali ya Wizara. Aidha, wataalamu wa Wizara washirikishwe kikamilifu katika hatua zote za uundwaji wa mfumo huo ili kuhakikisha wataalamu wa ndani wanapata ujuzi wa kutosha na kuweza kuusimamia na kuuendesha mfumo huo baada ya kukamilika kwake. Mfano wa mbinu hii imetumika na Baraza la Wawakilishi kupitia mfumo wa Baraza Mtandao (eHouse).

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa hatua hizi utaisaidia Serikali kujenga na kuimarisha uwezo wa wataalamu wa ndani katika kubuni, kuendesha na kusimamia mifumo ya TEHAMA kwa ufanisi na kuweza kujitegemea. Sambamba na hilo, utawezesha kufanyika kwa marekebisho ya haraka pale zinapojitokeza changamoto au hitilafu za kiufundi, pamoja na kurahisisha kuongeza, kupunguza au kuimarisha sehemu za mfumo (modules) au lango la huduma (portal) kulingana na mahitaji ya kiutendaji yanavyojitokeza kwa wakati. Aidha, hatua hizi zitapunguza utegemezi wa wataalamu wa nje na kuondoa vikwazo vya kupata ruhusa kutoka kwa kampuni au taasisi nyingine zinazomiliki mfumo, jambo litakaloongeza ufanisi katika utoaji wa

huduma, kuokoa muda na gharama, pamoja na kuimarisha usalama na kulinda usiri wa taarifa za Serikali.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuhitimisha, napenda kukushukuru kwa dhati kwa kunipatia fursa hii adhimu ya kuwasilisha hotuba ya Kamati ya Bajeti inayohusu majumuisho ya mjadala wa Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Aidha, natoa shukrani zangu kwa Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yao yenye kujenga na ushirikiano wao katika kufanikisha zoezi hili muhimu, ambao umewezesha kupatikana kufanyika majumuisho kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekee, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza, Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wengine wa Serikali kwa kuitikia wito wa Kamati na kushiriki kikamilifu katika vikao vyake. Ushirikiano wao na utoaji wa ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizoibuka uliiwezesha Kamati ya Bajeti kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na weledi.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa utulivu na usikivu wao wa hali ya juu wakati wa uwasilishaji wa hotuba hii ya Kamati ya Bajeti kuhusu majumuisho ya mjadala wa Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Uvumilivu na umakini wao umeonesha dhamira ya dhati ya kulinda maslahi ya wananchi na kuimarisha majadiliano yenye tija, jambo linaloendelea kujenga heshima na hadhi ya Baraza hili katika kutekeleza wajibu wake wa Kikatiba.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa, napenda kutumia fursa hii kuwakumbusha Mawaziri pamoja na Serikali kwa ujumla kwamba michango, maoni na hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe ndani ya Baraza hili tukufu hazikulenga kuikwamisha Serikali wala kupunguza jitihada zake za utekelezaji, bali zilikuwa na dhamira njema ya kuishauri, kuikosoa kwa kujenga na kusaidia kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Serikali ili Bajeti za Wizara zetu ziwe na tija, ufanisi na matokeo yanayoonekana kwa wananchi. Aidha, nawasisitiza Mawaziri wote kuhakikisha kwamba ahadi, maelekezo na maeneo yote mliyoyaahidi

kuyafanyia kazi wakati wa mijadala hii yanatekelezwa kwa vitendo, kwa uwazi na kwa wakati, ili kuendeleza imani ya wananchi kwa Serikali yao pamoja na kulipa heshima Baraza hili. Waheshimiwa Wajumbe wametumia muda, maarifa na uzoefu wao kutoa ushauri wenye manufaa makubwa kwa maendeleo ya nchi, hivyo utekelezaji wa hoja hizo utakuwa ni ishara ya kuthamini mchango wa Baraza na kuimarisha uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kusema hayo, nawashukuruni sana kwa kunisikiliza. Naomba kuwasilisha.

Ahsante,

…………..………

Mhe. Ali Suleiman Ameir,
Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**